Chuo Kikuu cha Sokoine
cha Kilimo

# MATUKIO YA SUA

*Januari - Machi, 2024*



**Ardhi ni Hazina**




*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda (kulia) na Mwakilishi wa WFP nchini Tanzania Bi. Sarah Gordon-Gibson (kushoto) wakitia saini Mkataba wa Ushirikiano*

# WFP na SUA kushirikiana kuhakikisha kunakuwa na usalama wa chakula

Shirika la Mpango wa Chakula Duniani Ukanda wa Tanzania (WFP) na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wamesaini Mkataba wa Ushirikiano ambao utasaidia tafiti, matumizi ya teknolojia ikiwemo Akili Mnemba na namna ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi.

Akizungumza Aprili 2, 2024 wakati wa utiaji saini makubaliano hayo Mwakilishi wa WFP nchini Tanzania Bi. Sarah Gordon-Gibson alisema mbali na maeneo hayo lakini pia Mkataba huo wa Ushirikiano utagusa maeneo mengine kama kubadilishana ujuzi na kuwajengea uwezo watafiti wa namna ya kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali.

Alisema WFP imetenga zaidi ya Dola za Marekani elfu 60 ambazo ni sawa na zaidi ya shilingi Milioni 150 za Tanzania kwa ajili ya SUA na wanaamini kuwa tafiti na uvumbuzi katika sekta ya kilimo na chakula ni kichocheo kikubwa cha mabadiliko katika sekta hiyo.

Bi. Sarah alisema ushirikiano baina ya SUA na WFP umekuja wakati mwafaka kwani utarahisisha na kuzipa msukumo tafiti za kisayansi, ameongeza kuwa kulingana na mpango mkakati wa WFP wa mwaka 2022 hadi 2027 na Ajenda ya Maendeleo Endelevu hadi ifikapo 2030, uvumbuzi uwe kielelezo muhimu cha kuhakikisha usalama wa chakula na lishe kwa watu wote.

Akizungumzia ushirikiano kati ya WFP na SUA, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda alisema SUA imefurahishwa na ushirikiano huo kwani utaongeza thamani katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na utafiti, uvumbuzi na teknolojia za kilimo.

Prof. Chibunda alisema katika kuhakikisha ushirikiano huo unakuwa imara SUA itafanya kazi bega kwa bega na WFP ili kuhakikisha inawasaidia wanataaluma, watafiti na wakulima kwa ujumla katika kuhakikisha usalama wa chakula na lishe.

Naye Mratibu wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalam SUA Dkt. Doreen Ndosi alisema ushirikiano huo wa WFP na SUA utatimiza ndoto ya Chuo hicho kuhakikisha usalama wa chakula kuanzia shambani, mavuno, uhifadhi, usafirishwaji kwa usalama na kumfikia mlaji wa mwisho kikiwa salama.

*Picha za matukio mbalimbali wakati na baada wa tukio la kusaini mkataba wa ushirikiano baina ya SUA na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani Ukanda wa Tanzania (WFP)*














# SUA yafundisha wanafunzi uvunaji salama wa misitu

*Wanafunzi wa mwaka wa kwanza, Shahada ya Misitu wakifuatilia mafunzo ya uvunaji salama wa mazao ya misitu*

*Katika kuhakikisha jamii inaondokana na uvunaji holela wa misitu kwa kutumia njia zisizo salama Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia Idara ya Uhandisi Misitu na Sayansi za mazao ya Misitu imetoa Mafunzo kwa Vitendo kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza, Shahada ya Misitu kuhusiana na uvunaji salama wa misitu hiyo lengo likiwa kuyatumia mafunzo hayo kutoa elimu kwa jamii.*

*Alisema hayo Bw. Ramadhani Sudi, Fundi Mchundo kutoka Idara ya Uhandisi Misitu na Sayansi za Mazao ya Misitu iliyopo Ndaki ya Misitu, Wanyamapori na Utalii kutoka SUA wakati akizungumza na SUAMEDIA kwenye Mafunzo hayo Kampasi ya Edward Moringe mjini Morogoro.*

*Alisema uvunaji holela wa misitu bila utaalamu unaweza kusababisha ulemavu na vifo hivyo wanapowafundisha wanafunzi wao kwa vitendo inawasaidia kujua uvunaji ulio salama na kuwafanya kuwa wafanisi na msaada mkubwa kwa jamii kwa kutoa elimu itakayosaidia jamii kuvuna kwa faida na salama kwa maendeleo endelevu.*

*Bw. Sudi aliwataka wanafunzi hao kuzingatia masomo na kufuata kile wanachofundishwa kwa lengo la kwenda kufanyia kazi kwa jamii inayowategemea kwa sababu jamii ina uhitaji mkubwa sana wa Mafunzo ya Misitu ili kuweza kufanya uvunaji salama wenye tija ndiyo maana wakati mwingine wanawaelekeza kupanda miti kibiashara kwa sababu mti ni faida.*

*Kwa upande wao Godbless Godson pamoja na Judith Sima wanafunzi wa mwaka wa kwanza Shahada ya Misitu SUA walisema kuwa wamekuwa na wiki takribani tano za Mafunzo kwa Vitendo ambayo kwa kiasi kikubwa yameonesha inahitajika elimu zaidi kwa njia ya vitendo na si nadharia pekee ili kuongeza ufanisi zaidi na lengo la Chuo ni kuhakikisha kile wanachojifunza wana uwezo wa kutoa na kukipeleka kwa jamii inayowazunguka lakini pia kuhakikisha jamii hiyo hiyo inatumia Rasilimali zinazowazunguka kwa ufanisi na ufasaha kutokana na elimu watakayoipata kutoka kwao kama wataalam wa misitu.*




# SUA yapokea magari mawili na vifaa vya kuendeleza kazi ya tafiti za misitu

***Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala Prof. Amandus Muhairwa (kulia) akipokea funguo za magari hayo toka kwa mwakilishi kutoka Forest Development Trust Bi Olive Luena mbele ya jengo la Utawala.***

*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Mipango, Fedha na Utawala Prof. Amandus Muhairwa ameongoza shughuli ya upokeaji wa Magari mawili pamoja na vifaa kwa ajili ya shughuli za utafiti wa misitu zinazofanywa na wataalamu chuoni hapo. Magari hayo mawili aina ya Toyota Hilux pick up pamoja na vifaa, vimetolewa na shirika la Forestry Development Trust (FDT) na vimepokelewa katika kampasi ya Edward Moringe, Morogoro.*

*Akizungumza kwa niaba ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Mipango, Fedha na Utawala, Rasi wa Ndaki ya Misitu Wanyamapori na Utalii Profesa Agnes Sirima, ameshukuru kwa kupokea magari hayo na kusema magari hayo ni matokeo ya mashirikiano waliyoingia mwishoni mwa mwaka 2023 na shirika la Gatsby Africa, ili kuendeleza utekelezaji wa mradi wa majaribio ya utafiti wa uboreshaji wa misitu 'Tree Improvement Research'.*

*Akizungumza baada ya kukabidhi magari hayo*
*Bi. Olive Luena muwakilishi toka Gatsby Africa pamoja na Forest Development Trust amesema kuwa, magari na vifaa hivyo vimetolewa kwa ajili ya maendeleo ya watanzania na wanafunzi wanaoendesha tafiti zao za misitu na wamechagua Chuo kikuu cha SUA kwa kuwa ni sehemu sahihi na pia kina mamlaka katika shughuli za utafiti wa mimea na misitu.*




## Ardhi ni Hazina

# SUA yashiriki Maadhimisho ya Kimataifa ya Siku ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi



*Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb) akihutubia wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimeshiriki katika maadhimisho ya siku ya kimataifa ya wanawake na wasichana katika Sayansi, ambayo kitaifa imeadhimishwa katika Mkoa wa Arusha siku ya Jumapili tarehe 11 Februari, 2024 na mgeni rasmi akiwa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb).

Mhe. Prof. Mkenda katika hotuba yake aliwaasa wasichana kujikita zaidi kwenye masomo ya sayansi na kuwahakikishia kuwa serikali ipo sambamba katika kuhakikisha wanapata elimu bora.

Aliongeza kuwa ulimwengu wa sasa umebadilika na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia yanakuwa kwa kasi pia, hivyo kama taifa linahitaji zaidi wasomi wa Sayansi na hivyo litaendelea kuwapatia motisha wanafunzi ili wapende kusoma masomo ya Sayansi, na wanaohitimu kupata fursa zaidi kutoka serikalini mfano Samia Scholarship ambayo serikali imekuwa ikiitoa kwa wanafunzi wanaofaulu masomo ya Sayansi.

Aidha Prof. Mkenda aliwataka wahadhiri wa vyuo kuwa walezi bora kwa wasichana na sio kuwa sababu ya kuwakatisha ndoto zao, hivyo kama serikali itaendelea kuwachukulia hatua kali wahadhiri watakapogundulika kuwa ni sababu ya kumkwamisha msichana.

Naye Mkuu wa Idara ya Lishe na Sayansi ya Mlaji na pia Mhadhiri Mwandamizi kutoka SUA Dkt. Hadija Mbwana alieleza kuwa SUA inaendelea kutoa nafasi kwa wasichana wa wanawake katika uongozi kwa kutoa kipaumbele kwenye nyadhifa za uongozi.

Aliongeza kuwa kwa upande wa wanafunzi wa kike wamekua wakiwapatia kipaumbele kwa kuwapa hosteli waingiapo chuoni. Lakini pia kuanzisha dawati la jinsia kwa lengo la kutoa uhuru na nafasi kwa wasichana na wanawake kupeleka malalamiko yao mbalimbali.

Maadhimisho hayo yalibebwa na kauli mbiu isemayo ‘Wanawake na wasichana katika uongozi wa Sayansi enzi mpya na maendeleo endelevu’ yamehudhuriwa na washiriki mbalimbali kutoka vyuo vikuu na vyuo vya kati, pamoja na wasichana mbalimbali kutoka katika shule za sekondari na msingi. lengo ni kumjenga mwanamke na msichana katika Sayansi na teknolojia.



# SUA, BAKITA na BAKIZA kushirikiana kusanifisha Istilahi za kilimo

Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) yamekubali pendekezo la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kushirikiana kusanifisha Istilahi za Kilimo.

Akizungumza na SUA Media Jijini Mbeya Machi 22, 2024 Katibu Mtendaji wa BAKITA Bi. Consolata Mushi alisema SUA wametoa wazo zuri na litasaidia kusaninifisha Istilahi za kilimo ili zitumiwe na wakulima.

Alisema fikra kuwa Sayansi haiwezi kuwa na Istilahi si sahihi kwa sababu BAKITA ina uwezo wa kusanifisha na imeshafanya hivyo kwa nyanja mbalimbali kama vile Hali ya Hewa, Mazingira, Benki, Sheria na wengine wengi.

Alisema wazo hilo la SUA ni mafanikio makubwa ya kukuza lugha ya Kiswahili ambayo hivi sasa inazungumzwa na zaidi ya watu milioni tano duniani kote.

Naye Katibu Mtendaji wa Baraza la Kiswahili Zanzibar, Dkt. Mwanaija Omary alisema ushirikiano baina ya BAKITA, BAKIZA na SUA utakuwa na manufaa makubwa kwani watu watatumia Msamiti fasaha na sanifu na Kiswahili kitazidi kuendelea.

Dkt. Mwanaija alisema SUA ni miongoni mwa Taasisi kubwa ya elimu nchini na inakuwa mfano wa kuigwa kwa wazo hilo ambalo litawasaidia wakulima kuwa na Msamiati fasaha katika mawasiliano kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Akizungumza wakati wa Kongamano la Nne la Idhaa za Kiswahili Duniani Dkt. Onesmo Nyinondi, mwakilishi wa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Prof. Raphael Chibunda alisema SUA inajiandaa kushirikiana na BAKITA na BAKIZA kuibua Misamiati ya kilimo.

Alisema pamoja na jitihada hizo chuo kinatumia vyombo vyake vya habari vya SUA Media ambayo inajumuisha Redio, Mitandao ya Kijamii au Sogozi na Televisheni kufikisha utafiti na uvumbuzi kwa lugha rahisi kwa hadhira.




*Dkt. Onesmo Nyinondi akifafanua namna SUA inavyoshiriki kukuza na kusambaza taarifa na ubunifu kwa jamii kwa kutumia lugha ya Kiswahili.*



*Wadau mbalimbali waliojitokeza katika Kongamano la Nne la Idhaa za Kiswahili Dunia lililofanyika Jijini Mbeya 22 Machi, 2024*

**Ardhi ni Hazina**

# SUA na Japani zasaini makubaliano ya kutekeleza Mradi wa Kudhibiti na Kuzuia Maambukizi ya Magonjwa



***Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala (kushoto) akitia saini Mkataba huo wa Makubaliano na mwakilishi mkazi wa Shirika la Maendeleo la Japani nchini Tanzania (JICA) Bw. Hitoshi ARA.***

*Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Shirika la Maendeleo la Japani (JICA) wamesaini Mkataba wa Makubaliano ya kutekeleza mradi unaojikita katika kudhibiti na kuzuia maambukizi ya magonjwa ambayo yanatoka kwa Wanyama kwenda kwa Binadamu au kutoka kwa Binadamu kwenda kwa Wanyama kwa kuzingatia magonjwa mawili ya kipaumbele ikiwemo Ugonjwa wa kutupa mimba (Brucellosis) na ugonjwa wa Kifua Kikuu au TB (Zoonotic Tubeculosis).*

*Zoezi hilo lilifanyika Februari 9, 2024 katika Kampasi ya Edward Moringe Sokoine mkoani Morogoro ambapo limeongozwa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo cha SUA, Prof. Raphael Chibunda.*

*Akizungumza na SUA Media baada ya kutia saini Mkataba huo wa makubaliano mwakilishi mkazi wa Shirika la Maendeleo la Japani nchini Tanzania (JICA) Bw. Hitoshi ARA- alisema mradi huo umelenga katika ufanyaji wa tafiti ambapo sehemu ya mwisho ya mradi huo watakubaliana kuanzisha timu moja kukabiliana na tatizo hilo, timu ambayo pekee itahusisha SUA, Serikali za mitaa Pamoja na taasisi mbalimbali na wanaamini kuwa kupitia mradi huo uhusiano wao na SUA utaimarika zaidi na zaidi.*

*"Napenda kuthamini mchango wa SUA kwa kuanzisha aina hii ya kazi vile vile aina hii ya mradi hivyo nisema historia baina ya JICA na SUA ni historia ya zaidi ya miaka hamsini (50) lakini tumekuwa tukilenga zaidi kwenye Sekta ya Kilimo pekee hivyo mradi huu unaokuja tumelenga katika mlengo wa AFYAMOJA ambayo inahusisha baina ya sekta mbalimbali au baina ya pande mbili katika udhibiti wa magonjwa hayo", alisema Bw. Hitoshi ARA-.*

*Kwa upande wake Rasi wa Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi Shirikishi SUA Prof. Esron Karimuribo, alisema Mradi huo unashirikisha Taasisi mbalimbali nchini na SUA ndio mwenyeji wa kutekeleza Mradi huo kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro lakini pia Taasisi ya Utafiti wa Tiba ya Wanyama na Tiba za Binadam (NIMR), Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi cha Muhimbili (MUHAS) na kwa upande wa Japan inaongozwa na Chuo Kikuu cha Rakuno Gakuen wakishirikiana na Taasisi nyingine za Elimu ya Juu Pamoja na Taasisi za Sekta binafsi.*





# Watumishi NMB watembelea SUA kupata elimu ya kilimo na ufugaji

Watumishi wa Benki ya NMB kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania ambao wanakaribia kustaafu wametembelea Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa lengo la kupata elimu, kujifunza kwa vitendo na kujionea shughuli mbalimbali za Kilimo na Ufugaji zinazofanywa Chuoni hapo ikiwa ni mojawapo ya maandalizi ya maisha baada ya kustaafu.

Program Meneja wa Kitengo cha Programu ya Ustawi wa Mwajiriwa kutoka Kampuni ya Assemble Insuarance ambaye ni Mratibu wa ziara hiyo John Ngonyani akizungumza siku ya Alhamisi Februari 8, 2024 alisema lengo kubwa ya ziara yao SUA ni kumuandaa mtumishi ambaye anajiandaa kustaafu aweze kuzitambua fursa mbalimbali zitakazompa mwangaza baada ya kustaafu.

"Tuna program ambayo inawaandaa wastaafu wafanyakazi kwa ajili ya kustaafu na mara nyingi tunachukua watu ambao wamekaribia kustaafu kuanzia miaka 45-50, mafunzo haya yanalenga sana kuwawezesha kuingia kwenye ujasiriamali kwa maana kwamba wengi ni waajiriwa na wengi wamejaribu kufanya biashara lakini wakashindwa vile vile wamewahi kulima lakini wakakwama hivyo sisi tunalenga zaidi kuwakwamua pale waliposhindwa ili wasogee mbele", alisema Bw. Ngonyani

Alisema wameichagua SUA kama sehemu ya kujifunzia kwa kuwa ndio kitovu cha Kilimo nchini na wanaamini watumishi hao kwa sababu wanaenda kwenye kustaafu na sehemu pekee ambapo wanaweza kuwekeza kirahisi ni kwenye kilimo ikiwemo kwenye Ufugaji wa Samaki, Ngombe wa maziwa, kuku, kilimo cha matunda na mbogamboga ambavyo havihitaji nguvu nyingi hivyo kwa mtu ambaye ni mstaafu inakuwa ni rahisi kwake kufanya vitu hivyo na kuweza kujikwamua kiuchumi.

Kwa upande wao wastaafu hao watarajiwa Kizito Shija Mtaalam wa Majengo wa NMB kutoka Ofisi za Kanda Dodoma na Atupele Lunkombe Afisa wa Benki NMB kutoka Simiyu waliwashukuru Wataalam wa SUA kwa kuwapatia elimu na maarifa ya kutosha ambayo yamewachochea katika akili zao kuwa wakistaafu wanaweza kujiingiza katika shughuli mbalimbali za kilimo ambazo zitawasaidia kuwaingizia kipato na kujikimu kimaisha hivyo imewaondoa hofu ya kustaafu na kuwapelekea wengi wao kutamani kustaafu hata kabla ya wakati na kuingia kwenye ujasiriamali kwa sababu ya SUA.

Katika ziara hiyo Watumishi hao walitembelea Shamba la Mafunzo katika Kitengo cha Uchumi wa Buluu, Kitengo cha Wanyama na Kitengo cha Bustani na Mbogamboga kinachojihusisha na uzalishaji wa Mbogamboga na matunda, Miche ya viungo mbalimbali pamoja na Maua.

**Ardhi ni Hazina**

# Ushirikiano wa SUA na Chuo Kikuu cha Artemisa cha Cuba utainua taaluma, ujuzi na kunufaisha wananchi - Dkt Bermundez




***Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda (kulia) na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Artemisa Dkt. Adianez Bermundes (kushoto) wakitia saini Hati ya Makubaliano (Picha kwa hisani ya Ofisi ya Makamu wa Rais).***

Imeelezwa kuwa ushirikiano ulioanzishwa kati ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Chuo Kikuu cha Artemisa cha Jamhuri ya Cuba utakuwa na manufaa makubwa baina ya vyuo vikuu hivyo kwani utainua taaluma, ujuzi na kunufaisha wananchi wa pande zote mbili yaani Tanzania na Cuba.

Akizungumza na viongozi mbalimbali wa Manejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Januari 25, 2024. Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Artemisa Dkt. Adianez Bermundes alisema mahusiano baina ya pande hizo mbili yatawajengea uzoefu, ujuzi na taaluma wanafunzi na wanataaluma kwa kubadilishana uzoefu, teknolojia na kufanya utafiti mbalimbali.

Alitolea mfano mazao ya mihogo, viazi na magimbi kuwa ni baadhi ya mazao ambayo yamefanyiwa na yanaendelea kufanyiwa tafiti katika Chuo Kikuu cha Artemisa ili kuona ni kwa namna gani watu wanaweza kuendelea kuyatumia huku wakichanganya na vyakula vingine ili kuondoa hali ya kutegemea kula chakula cha aina moja.

Akizungumzia namna ya kuinua hali za wakulima katika maeneo ya nchi Dkt. Bermundez alisema chuo chao kimekuwa kikitoa elimu ya moja kwa moja kwa wazalishaji wa mazao jambo ambalo limekuwa na mafanikio makubwa pamoja na kuwa nchi yao imekuwa katika vikwazo mbalimbali kwa muda mrefu lakini imejimudu kwa kuwa na chakula cha kutosha.

Katika hatua nyingine, alitoa ahadi kwa SUA kuwa atakiunganisha chuo hicho na vyuo vingine vinavyotoa elimu inayolingana na ile wanayoitoa SUA ili kuleta ufanisi zaidi kwa Tanzania lakini pia kwa Cuba.

Awali akimkaribisha Dkt. Bermundez Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda alisema Januari 24, 2024 SUA na Chuo Kikuu cha Artemisa vilitia saini Hati ya Makubaliano baina ya pande hizo mbili mbele ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania Mhe. Philipo Mpango na Makamu wa Rais wa Cuba Mhe Salvador Veldas Mesa .

Aidha Prof. Chibunda alimshukuru Dkt. Bermundez kwa kukubali kualika ujumbe kutoka SUA kwenda nchini humo mapema mwaka huu ili kuona ni kwa namna gani pande hizi mbili zitanufaika na ushirikiano huo.

Dkt. Bermundez pia alipata wasaa wa kujua mambo mbalimbali yaliyopo SUA ambapo katika wasilisho lake Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala alisema chuo kimekuwa na mafanikio makubwa tangia kuanzishwa.

Akitoa neno la shukrani kwa ujio wa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Artemisa cha Cuba, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Mipango, Utawala na Fedha Prof. Amandus Muhairwa alisema ushirikiano baina ya Tanzania na Cuba ni wa kihistoria na anatarajia ushirikiano baina ya SUA na Artemisa utaleta matunda makubwa si kwa vyuo hivyo pekee lakini kwa wanachi wote.

Akiwa Chuoni hapo Dkt. Bermundez ametembelea maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Wanyama iliyopo SUA.

*Picha za matukio mbalimbali ya ziara ya Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Artemisa cha nchini Cuba Dkt. Adianez Bermundes.*













# SUA, JKUAT kuendelea kubadilishana uzoefu na maarifa

*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala (katikati, waliokaa) , Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Mipango, Fedha na Utawala Prof. Amandus Muhairwa na Naibu Makamu Mkuu Taaluma kutoka JKUAT Professa Robert Kinyua wakiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wengine wa SUA ana JICA.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Chuo Kikuu cha Jomo Kenyatta cha Kilimo na Teknolojia (JKUAT) kuendeleza mashirikiano kwa lengo la kubadilishana wanataaluma, wanafunzi, kushirikiana katika tafiti za kilimo na uhandisi ili kubadilishana uzoefu na maarifa.

Rasi wa Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi Shirikishi, SUA Prof. Esron Karimuribo, alisema kuwa vyuo hivyo vimedumisha mashirikiano hayo takribani miaka kumi kwa sasa wapo katika mchakato wa kufanya mashirikiano hayo kuwa rasmi na kuongeza miaka mitano kuendelea kujikita katika kutengeneza mitaala, kufundisha kwa pamoja katika sekta mbalimbali na tafiti na bunifu.

Pamoja na mambo mengine Prof. Karimuribo ameongeza kuwa makubaliano hayo yaahusu pia matumizi ya teknolojia ya kisasa ya akili bandia (Artificial Intelligence) katika fani za uhandisi na mabadiliko ya tabia nchi na kujikita katika sayansi ya majini (Marine Sciences).

Kwa upande wao Naibu Makamu Mkuu Taaluma kutoka JKUAT Professa Robert Kinyua, na Mratibu wa Mradi kutoka Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA) Mai Toda Nakano, wamesema kuwa ushirikiano huo utakuwa mahususi kwa ajiri ya kuunda mtandao wa Elimu ya juu na kuwezesha wanafunzi kujifunza kutoka sehemu mbalimbali kwa pamoja.





# Mfumo mpya wa Kidijitali wa Malipo wawasaidia Wanafunzi SUA kupata fedha kwa wakati



*Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wameishukuru Bodi ya Mikopo kwa kuwarahisishia kupata fedha za kujikimu na matumizi kwa wakati kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ambapo imewezesha wanafunzi hao kuendelea na masomo kwa wakati Chuoni hapo.*

*Akizungumza na Kitengo cha Mawasiliano na Masoko katika mahojiano yaliyofanyika Chuoni hapo, Mhasibu na Afisa Mikopo wa Dawati la Mikopo la Elimu ya Juu kutoka SUA Frida Malya, alisema wanaendelea na zoezi la kuwasajili wanafunzi wanufaika katika Mfumo mpya wa Kidijitali wa Malipo (Digital Disbursement Solution – DiDiS ) wakisaidiana na Maafisa kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.*

*Aidha Malya alisema kuwa mfumo huo ulioboreshwa utasaidia wanufaika kuachana na mfumo wa kusaini pesa kwenye makaratasi badala yake watapata fedha za kujikimu ndani ya saa 24 baada ya kutumiwa ujumbe wa kuingiziwa pesa kutoka Bodi ya Mikopo.*

*Kwa upande wake Afisa Mikopo Daraja la Pili kutoka HESLB Edward Kilele alieleza kuwa mfumo huu wa DiDiS ni mfumo wa Kidigitali ambapo mnufaika atatumia mfumo wa Student's Individual Permanent Account (SIPA) kuangalia mgawanyo, na itasaidia kupunguza adha ya foleni kwa wanafunzi, pia itasaidia Bodi ya Mikopo kufanya ufuatiliaji wa fedha hizo na amesema kuwa wanafunzi wanaweza kupata fedha kwa kupakuwa application ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu yaani 'HESLB App'.*

*"Tunaishukuru sana Serikali kwa ufadhili huu wa fedha pia naishukuru Bodi ya Mikopo kwa kugundua mfumo mpya wa DiDiS ambao umerahisisha kupata fedha za kujikimu na matumizi kwa urahisi tofauti na zamani ambapo pesa zikitoka tunapanga foleni, lakini kwa sasa tunaweza kupata fedha popote tulipo na kwa wakati, pia nawashauri wanafunzi wenzangu tutumie fedha vizuri ili tuendelee kufaidika na ufadhili huu", alisema Albertina Kihundwa, Mwanafunzi wa Mwaka wa Pili wa Stashahada ya Kwanza ya Udaktari wa Wanyama Chuo cha SUA.*

*Kwa upande wao Ruth Msechu, anayesoma Kozi ya Kilimo na Antony Michael Kozi ya Shahada ya Uuguzi wa Wanyama wote wakiwa ni wanafunzi wa mwaka wa pili SUA waliishukuru Serikali kupitia Bodi ya Mikopo kwa kuruhusu mfumo huo mpya ambao umesaidia wanafunzi kujihudumia wenyewe na hivyo kuwawezesha kuanza masomo kwa wakati. Mfumo huu wa DiDiS unalenga kusajili wanafunzi waliopata mkopo kwa mara ya kwanza katika mwaka wa masomo 2022/2023 waliopo katika Taasisi zote za Elimu ya Juu nchini, usajili utakapokamilika wanafunzi wote wanufaika wa mikopo waliopo vyuoni wapatao 202,016 watakuwa wanapokea fedha kupitia DiDiS.*



***Mhasibu na Afisa Mikopo wa Dawati la Mikopo la Elimu ya Juu kutoka SUA Bi. Frida Malya akizungumza na wanahabari, (hawaonekani pichani)***

# SUA yaendelea kuboresha programu za Chuo



Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia Kurugenzi ya Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalam kwa siku mbili mfululizo kimeendelea kufanya mapitio ya Programu zao za Shahada za Uzamili kwa lengo la kuziboresha ili ziwe na uwezo wa kuyafikia mahitaji ya jamii ya watanzania.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Uzamili, Utafiti, Uhaulishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalam Prof. Japhet Kashaigili wakati akizungumza na SUA Media ambapo amesema wamekuwa wakifanya mapitio hayo ya Mitaala chini ya Program ya HEET ambayo imewawezesha kuangalia Mitaala yao iko kwenye hali gani kwa sasa ukilinganisha na uhalisia wa soko ili waweze kuiboresha na kufikia matakwa ya soko ambapo ni jambo la msingi katika kuleta manufaa yenye tija.

Alisema mapitio hayo yamefanywa na wataalam wa Chuo lakini pia yamewahusisha wadau mbalimbali ambao ni wanafunzi waliohitimu Chuoni hapo, wadau kutoka taasisi mbalimbali za kiserikali pamoja na za umma na watu binafsi ambao wanavutiwa na program zinazotolewa na SUA na kwamba zoezi hilo ni la msingi kwa kuwa linawawezesha kujua aina ya program walizonazo na zinahitaji nini ili kuweza kuwa na mvuto zaidi na hivyo kuweza kupata wanafunzi wengi kwenye Chuo hicho.

"Kwa hiyo hili ni zoezi muhimu sana kwa sababu linaonesha mustakabali wa Chuo kwa maana ya kwamba wanafunzi ambao watakuja chuoni kwetu lakini pia matumizi ya wale wahitimu wetu ni wapi wanaweza wakaajiriwa hivyo suala hili linaandaliwa kwa ajili ya kujenga maendeleo ya ujuzi kwenye suala zima la uandaaji wa hizi program ambazo tumekuwa tukiendelea kuzipitia", alisema Prof. Kashaigili.

Aidha alisema licha ya kufanyia maboresho program zilizo kuwepo vile vile wanaanzisha program zingine mpya kulingana na hitaji la soko kwa sasa ikiwemo kuingiza masuala ya namna ya kutumia akili bandia (Artificial Inteligency) kwenye masuala ya uzalishaji na masuala mtambuka ambayo yanaendana na soko la sasa.

Kwa upande wake Dkt. Zahra Majili alisema wanacholenga ni kuhakikisha Mitaala yao inaweza kuendana moja kwa moja na soko la ajira lakini pia hali halisi ya muhitimu anayetoka SUA kuweza kuwa na uwezo wa kupata kazi kwa haraka iwe kwa kuajiriwa au kujiajiri hivyo wanahitaji elimu ambayo itawafanya wadau wao ambao ni wanafunzi iweze kuchangia katika kuhamasisha ukuaji wa uchumi wa nchi.

Naye mmoja wa wanafunzi walioshiriki katika zoezi hilo Rafiki Hamza alisema kuwa manufaa makubwa ya zoezi hilo ni kuwa Mitaala hiyo inalenga kutengeneza wahitimu watakaoenda kuuzika kwenye soko la ajira wakiwa na ujuzi ambao unahitajika kuendana na mabadiliko ya Kiteknolojia lakini pia mifumo ya kijamii.



**Ardhi ni Hazina**



# SUAMEDIA yashiriki Mkutano wa Mwaka wa Vyombo vya Utangazaji nchini

Rai imetolewa kwa vyombo vya habari nchini kuwa na vipindi maalum vitakavyohamasisha jamii kuzijua mila na desturi za kitanzania ili kujenga taifa lenye maadili na uzalendo ambao ndio chachu ya maendeleo ya taifa.

Rai hiyo ilitolewa Februari 13, 2024 na Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhandisi Kundo Mathew wakati akifungua Mkutano wa Mwaka wa Vyombo vya Utangazaji nchini ikiwemo unaofanyika jijini Dodoma.

Mhandisi Mathew alisema pamoja na mafanikio makubwa yanayotokana na uwepo wa vyombo vya habari kuweza kuifikia jamii kirahisi zaidi lakini kumekuwa na changamoto ya baadhi ya vyombo hivyo kukiuka kanuni za utangazaji hali inayochangia kuwepo kwa mmomonyoko wa maadili nchini.

“Sekta ya habari imekumbwa na mabadiliko ya Teknolojia na hivyo kuathirika na utandawazi uliopo, sisi sio kisiwa lakini pamoja na hayo Serikali inaendelea kufuatilia na kuchukua hatua stahiki ikiwa ni sanjari na kutoa elimu kwa vyombo hivyo ili kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko hayo ya teknolojia”, alisema Mhandisi Mathew.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri huyo aliwataka washiriki waliohudhuria mkutano huo kuzielewa ipasavyo Kanuni za uchaguzi zinazotumika nchini ili uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu pamoja na Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwakani uwe wa amani na mafanikio makubwa.

Miongoni mwa mada zinazojadiliwa katika mkutano huo ni Hali ya Maadili na Matumizi ya Taaluma ya Utangazaji nchini, Hali ya Maadili na Matumizi ya Taaluma ya Utangazaji kwenye mitandao ya kijamii, Matumizi bora ya mitandao ya kijamii kwa watengeneza maudhui, pamoja na matumizi ya kazi za Sanaa na Filamu kwenye vyombo vya Utangazaji.

SUA Media ilishiriki katika Mkutano huo uliofanyika kwa siku mbili jijini Dodoma ambao umebeba Kauli Mbiu isemayo “ Maadili na Taaluma ya Utangazaji".





# Watumishi Kampasi ya Mizengo Pinda hakikisheni mnaaminika kazini - Prof. Mahonge



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kuthibiti Uadilifu SUA Prof. Christopher Mahonge aliyekaa (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda, wa pili kutoka kushoto waliokaa ni Naibu Rasi wa Kampasi ya Mizengo Pinda Mipango, Utawala na Fedha Prof. Jeremiah Makindara.*

Watumishi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wametakiwa kuhakikisha wanaaminika na kutegemeana katika utumishi wao ili kuleta tija na ufanisi kazini.

Akizungumza na watumishi wa SUA Kampasi ya Mizengo Pinda iliyoko Wilayani Mlele Mkoani Katavi hivi karibuni, Mwenyekiti wa Kamati ya Kuthibiti Uadilifu SUA Prof. Christopher Mahonge alisema kuna baadhi ya watumishi wamekuwa na changamoto ya kukosa uaminifu na kushindwa kufikia malengo ya taasisi.

Alisema mtumishi anapokuwa ni mwaminifu na tegemeo katika kazi yake inaisaidia Taasisi kuwa na uhakika kuwa jakumu aliyopangiwa mtumishi yatatekelezwa kwa wakati na kusaidia Taasisi kufikia malengo yake.

Prof. Mahonge alisema watumishi wanapokuwa katika eneo moja mahusiano si yale mazuri pekee kwani kuna wakati watumishi hutofautia lakini cha kujiuliza ni je mara baada ya kutofautiana nini kinafanyika baadae ili kuhakikisha Taasisi inaenda kwa pamoja.

Awali akimkaribisha Mwenyekiti wa KKU – SUA ili kuzungumza na wafanyakazi wa Kampasi ya Mizengo Pinda, Naibu Rasi wa Kampasi ya Mizengo Pinda Mipango, Utawala na Fedha Prof. Jeremiah Makindara alisema KKU inafanyakazi nzuri katika kuhakikisha watumishi wanajua wajibu wao katika kazi.

Alisema ni wajibu wa watumishi kuzingatia uadilifu kazini na katika jamii kama inavyoelezwa au kufafanuliwa na kamati hiyo kwani huo ndiyo mwongozo wa utumishi wa umma.



*Picha ya juu na ya chini ni baadhi ya Watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda wakifuatilia kwa umakini hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuthibiti Uadilifu SUA Prof. Christopher Mahonge (haonekani pichani)*



**Ardhi ni Hazina**

# 'SUA tumieni wabunifu, katika kukuza mazao ya kimkakati'



***Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Malima akizungumza na vijana wabunifu (hawaonekani pichani) wakati akizindua shindano la vijana la kuwezesha ubunifu na kampuni changa za kiteknolojia ya kilimo Tanzania.***

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Malima amewahimiza vijana wenye bunifu mbalimbali kuendelea kutumia maarifa yao katika kubuni teknolojia mbalimbali ambazo zitawasaidia wakulima kulima kisasa na kuongeza thamani ya shughuli zao.

Amesema hayo wakati akizindua Shindano la uwasilishaji wa wazo la kibunifu linalohusisha teknolojia kwa mkoa wa Morogoro ambalo limefanyika katika Hoteli ya Morena iliyopo mkoani hapa Februari 19, 2024 kwa kufadhiliwa na Mradi wa YEESI LAB SUA.

Katika kinyang`anyiro hicho vijana saba kati ya 100 ndiyo walioingia fainali kabla ya kupatikana mshindi mmoja ambaye kupitia mradi huo atapatiwa ufadhili wa kuendelezwa zaidi katika wazo husika.

Mhe. Malima amesema amesikiliza bunifu za vijana hao na kuona endapo zitaenda katika utekelezaji zitakuwa na tija kwa wananchi wengi wa mkoa huo kwani kumekuwa na mwendelezo wa wakulima kulima kimazoea.

Hata hivyo, ametoa shime kwa vijana hao kuendelea kubuni mawazo bunifu zaidi ili wakulima wainuke kiuchumi kupitia shughuli za kilimo.

“Naamini haya mawazo yakienda kwenye utekelezaji wakulima watalima kwa tija, na watanzania wengi wataingia kwenye shughuli za kilimo wakiachana na mawazo ya kuona kujihusisha na kilimo ni kushindwa maisha”, alisema.

Mwakilishi wa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Esron Karimuribo amesema vijana hao wabunifu wanatoka mkoa wa Morogoro na bunifu zao zinalenga katika mkoa huo.

Amesema SUA miaka 15 iliyopita haikutoa kipaumbele katika bunifu kama ilivyo sasa ambapo imekuwa ikihimiza watu kufanya tafiti ambazo zitakuja na majibu ya changamoto kwenye jamii.

Mwakilishi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mkurugenzi Msaidizi anayehusika na Sayansi na Teknolojia Dkt. Alexander Mtawa amesema kama Wizara itaendelea kuunga mkono taasisi za serikali na binafsi ambazo zinajikita katika bunifu chanya kwa jamii, akisema bunifu hizo wao wanaamini zitasaidia kuondoa matatizo kwa wananchi.

Mkuu wa Mradi wa YEESI LAB Dkt. Kadeghe Fue amesema vijana hao wabunifu watasaidiwa kufungua kampuni na masuala yote ya uendeshaji ndani ya mkoa wa Morogoro.





**Ardhi ni Hazina**

# Wizara ya Kilimo yaipongeza SUA kupitia watafiti wake kwa Tafiti nzuri za Kilimo



*Mkurugenzi wa Idara ya Mafunzo huduma za ugani na utafiti Dkt. Wilhelm Leornad Mafuru wakati akifungua Mkutano huo wa Mradi wa TRADE HUB.*

Wizara ya Kilimo imekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo (SUA) kupitia wataalamu wake kwa namna kinavyofanya Tafiti nzuri na muhimu ambazo zinasaidia Taifa katika kufanya maamuzi muhimu kwenye sekta ya kilimo pamoja na kutatua changamoto mbalimbali za wakulima ili kuinua uchumi wa jamii na nchi.

Pongezi hizo zilitolewa na Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe (MB) Kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Idara ya Mafunzo huduma za ugani na utafiti Dkt. Wilhelm Leornad Mafuru wakati akifungua Mkutano wa uwasilishwaji wa matokeo ya Mradi wa Biashara, Maendeleo na Mazingira nchini TRADE HUB unaofanyika Jijini Dodoma na kuwakutanisha wadau wote walioshiriki kwenye mradi huo wa miaka mitano.

"Sisi sote ni mashuhuda ya mchango mkubwa wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo katika kusaidia kuboresha kilimo chetu nchini, tumesikia shuhuda mbalimbali humu za mtu mmoja mmoja lakini pia za wadau ikiwemo mashirika na vikundi na hii inatufanya kuamini kuwa Chuo hiki kinatoa mchango uliotukuka" alisema Dkt. Mafuru.

Alisema mradi huu wa TRADE HUB umetekelezwa katika wakati muafaka ambao nchi inatekeleza sera ya kuinua uchumi kupitia sekta za Kilimo,Viwanda na Biashara hivyo matekeo ya mradi huu yatasaidia katika kufanikisha mpango na mkakati huo kupitia kufanya maamuzi yanayotokana na utafiti wa kisayansi.

Dkt. Mafuru alisema matokeo ya mradi huo yatasaidia kuongeza ubunifu katika mnyororo mzima wa thamani wa uchakataji wa bidhaa na kuziongezea thamani na hatimae kuongeza kipato cha wananchi na kuipatia serikali mapato.

Akitoa salamu za Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Upande wa Taaluma Utafiti na ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala alisema mradi huo ni sehemu tuu ya miradi mingi ambayo inasaidia nchi kufikia malengo yake kwa kupata ushahidi wa kisayansi kwenye sekta mbalimbali.

Prof. Mwatawala alisema ni matumaini yake kuwa matokeo ya utafiti huo yatasaidia wizara katika kuboresha sera zilizopo na kutunga zingine ambazo zitawezesha uzalishaji na uuzaji wa mazao hayo katika soko la ndani na lile la kimataifa na kusaidia Taifa kujipatia fedha na kuinua uchumi.

Mradi huo unatekelezwa na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha sokoine cha Kilimo kwa kwa kushirikiana na washirika wa Maendeleo kutoka nchi 15 za Afrika, Asia, Ulaya na Amerika ya Kusini kwa ufadhili wa Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP).



*Picha ya pamoja ya mgeni rasmi, Viongozi wa SUA pamoja na wadau walioshiriki mkutano huo kutoka Taasisi na maeneo mbalimbali nchini.*

**Ardhi ni Hazina**

# SUA kuingia makubaliano na Chuo cha China ZZULI



*Picha ya pamoja Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala (katikati waliokaa), Makamu Mkurugenzi wa Taaluma kutoka Zhengzhou Bw. Wang Jiwei (kulia) na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Amandus Muhairwa (kushoto) pamoja na Watumishi wengine wa SUA na kutoka China.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Chuo Kikuu cha Zhengzhou cha nchini China (Zhengzhou University of Light Industry (ZZULI) vimekubaliana kuingia kwenye makubaliano ya awali ya jumla ili kutengeneza ushirikiano wa masuala mahususi katika siku zijazo.

Hayo yamefikiwa baada ya SUA kuupokea ugeni wa Chuo cha Zhengzhou cha nchini humo kikiwa na lengo la kutazama maeneo ambayo taasisi hizo mbili zinaweza kushirikiana kwa manufaa ya taifa na kuendeleza historia iliyopo baina ya Tanzania na China.

Akizungumza na Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Februari 23, 2024 wakati wa ziara hiyo, Makamu Mkurugenzi wa Taaluma kutoka Zhengzhou Bw. Wang Jiwei amesema kutokana na wasilisho la Naibu Makamu wa Chuo ameona baadhi ya maeneo ambayo pia katika Chuo chao wanafanya ikiwemo masuala ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kutumia teknolojia ya kisasa, akiongeza kwa kuwakaribisha wawakilishi wa SUA kupanga ziara ya kwenda kutembelea na kujionea uendeshaji wa taasisi hiyo ya elimu juu yenye zaidi ya Wanafunzi 30,000.

Kwa upande wake Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda amesema anakishukuru Chuo kwa kupanga ziara ya kufika SUA, akisema huo unakuwa mwanzo wa kushirikiana.

Aidha, Prof. Mwatawala amekishukuru Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM) kwa kuonesha ushirikiano mkubwa katika kuhakikisha ugeni huo unafika SUA baada ya awali ugeni huo kupokelewa katika Chuo cha MUM.

Baadhi ya mambo ambayo wamesema wanaweza kushirikiana kwa kuingia kwenye mkataba wa maelewano (MoU) ni katika





# Wataalam wa Tiba ya Wanyama Tanzania Bara na Visiwani wakutana SUA

Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi limeendesha mafunzo kwa wataalam wa tiba ya wanyama wa Tanzania Bara na Visiwani katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa lengo la kukabiliana na magonjwa ya mlipuko kwa wanyama.

Mafunzo hayo ambayo yalifunguliwa na Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania Dkt. Benezeth Lutegemalinda yatakuwa mafunzo ya muda wa miezi minne ambapo mwezi mmoja washiriki wa mafunzo hayo watayatumia darasani na miezi mitatu katika maeneo wanayofanyia kazi.

Dkt Lutegemalinda alisema malengo ya mafunzo hayo yanawataka washiriki kushiriki vyema ili kwenda kuisaidia jamii kwani mafuno hayo yametumia gharama kubwa hivyo ni vyema kila mshiriki akapata kile kilichokusudiwa. Pia kuisaidia sekta ya mifugo katika maeneo yao ya kazi kwa kwenda kuwafundisha wengine walio chini yao na walio katika idara zao ofisini.

Aliongeza kuwa Wizara inategemea washiriki hao ambao ni watumishi wa serikali kwenda kupunguza magonjwa ya wanyama na magonjwa yanayotoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu ili kuhakikisha ile asilimia ya sasa ambayo ni 60 ya maambukizi ya magonjwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu inafutika na kuwa asilimia sifuri.

Aidha alilishukuru Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa kwa kuendelea kushirikiana na serikali kwa lengo la kutoa mafunzo kwa wataalam waliopo makazini ili kusaidia jamii wanazozitumikia.

Kwa upande wake mwakilishi wa Shirika hilo Bi. Stella Kiambi aliwapongeza washiriki wote kutoka Tanzania Bara na Visiwani kwa kujitokeza katika mafunzo hayo na kuwa mafunzo hayo ni muendelezo wa mafunzo ambayo yataendelea kutolewa kwa wataalam mbalimbali kwa kushirikiana na Serikali.

Mafunzo hayo yaliyofanyika katika ukumbi wa ICE ulipo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo yalishirikisha washiriki kutoka Mikoa na Wilaya mbalimbali za Tanzania Bara na Visiwani.





# SUA kuboresha vitendea kazi Idara ya Sayansi ya Udongo na Jiolojia

Maabara ya Sayansi ya Udongo, Idara ya Sayansi za Udongo na Jiolojia ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo imenunua na kukarabati vifaa vya upimaji udongo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji katika sekta ya Kilimo.

Hayo yalibainisha na Mkuu wa Maabara ya Sayansi za Udongo kutoka Idara ya Sayansi za Udongo na Jiolojia SUA Amour Suleimani ambapo amesema kupitia Mradi fedha zipatazo milioni 400 zimetolewa na Miradi ya Utafiti kutoka Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

Alisema mashine kubwa mbili ikiwemo **Microwave Digestor** pamoja na **ICP OES (Inductively Coupled Plasma Optical Emission Spectroscopy)** na kuweza kukarabati mashine yao kubwa ambayo imekuwa haifanyi kazi kwa muda mrefu iitwayo **AAS (Atomic Absoption Spectiometer).**

Amour Suleiman alisema wamebadilisha mfumo wa kieletroniki kwa maana ya kununua vifaa vya kieletroniki na programu wanazotumia katika usajili wa sampuli lakini pia upatikanaji wa data hivyo kuboresha mfumo mzima wa utoaji majibu na pia uhifadhi wa taarifa za wateja wao.

Bw. Suleiman alisema **Microwave Digestor** waliyonunua ina uwezo wa kuchakata sampuli ishirini na nne (24) kwa muda wa dakika 50 ambapo hapo awali walikuwa wakitumia mfumo wa **Open System/Digest System** ambao ulikuwa unawaruhusu kuchakata sampuli ishirini (20) kwa siku tatu.

"Maabara yetu kwa sasa imekuwa na ufanisi mkubwa zaidi ukilinganisha na awali hivyo nipende kuwakaribisha wadau mbalimbali wakiwemo wakulima wadogowadogo, wakati, wakubwa lakini pia makampuni kutumia maaba ajili ya upimaji wa sampuli, maji, mbolea na mimea kabla ya kuanza kuzitumia mashambani", alieleza Amour Suleiman.



Kaimu Rasi wa ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo CoNAS Dkt. Beda Mwang'onde wakati akifungua mafunzo hayo.

# CoNAS yawajengea uwezo Wanafunzi wa Shahada za Juu namna ya kuandika maandiko ya kisayansi ili yalete tija kwa Taifa.

Wanafunzi wa shahada za juu wa kozi mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wametakiwa kuhakikisha wanafanya utafiti kwa kufuata misingi na taratibu zote za kisayansi kuanzia kukusanya taarifa,uchakataji na uchapishaji kwenye majarida sahihi ili ziweze kusaidi jamii na taifa katika kufanya maamuzi sahihi ya kisayansi.

Wito huo umetolewa na Kaimu Rasi wa Ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo CoNAS Dkt. Beda Mwang'onde wakati akifungua mafunzo ya siku mbili yaliyoandaliwa na Ndaki hiyo kwa lengo la kuwajenga uwezo wanafunzi katika kuandaa maandiko ya kisayansi.

"Lazima tufahamu kuwa pamoja na kwamba tufanya utafiti kama wanafunzi kutimiza vigezo vya kupata shahada zetu lakini tufanya tafiti ili kutatua changamoto tulizonazo kwenye jamii hivyo ni muhimu sana kufuata kanuni na taratibu za kisayansi kwenye mchakato mzima wa ufanyaji wa utafiti wetu kwakuwa utafiti huo unatumiwa na jamii na taifa hivyo tukipika matokeo tunaweza kusababisha madhara kwa watumiaji wa taarifa hizo kwakuwa tutakuwa tumewapotosha" alisisitiza Dkt. Beda.

Amewataka kuhakikisha matokeo ya Utafiti wao unachapishwa kwenye majarida sahihi ya kisayansi ili yaweze kutumiwa kimataifa lakini pia kuwatumia vyema wasimamizi wao katika kuchagua majarida hayo ili kuepuka kuchapisha kwenye majarida yasiyo na sifa na kupeleka kuingia kwenye migogoro na Chuo kwa kuchapisha kwenye majarida yasiyokubalika na Chuo.

Awali akizungumzia lengo la mafunzo hayo mratibu wa mafunzo ambaye pia ni Mratibu wa Shahada za Juu katika ndaki hiyo Dkt. Alcardo Alex Barakabitze amesema ni kuwajengea uwezo wanafunzi wa shahada za Uzamivu, uzamili na watafiti wachanga katika kuandika maandiko ya kitaaluma.

"Lengo la mafunzo haya ya siku mbili ni kuwajengea uwezo wanafunzi wa Uzamili,Uzamivu na watafiti wachanga namna ya kuandika maandiko ya kisayansi na uchapishaji wa kazi zao ili zichangie kikamilifu kwenye kuzalisha maarifa lakini pia kujenga ushirikiano endelevu kati ya wanafunzi hao na wa kwenye Taasisi zingine Afrika sambamba na mbinu za uandishi wa maandiko ya kuomba fedha za miradi ya utafiti" alifafanua Mratibu Dkt. Alcardo.

Akiwasilisha mada yake kuhusu utengenezaji wa ushahidi wakisayansi na uandaaji wa maandiko madogo ya sera kwaajili ya watunga sera Prof. Faith Mabiki amesema pamoja na wanafunzi hao kuchapisha kwenye majarida ya kimataifa ni muhimu pia kuandaa maandiko madogo ya kisera kwaajili ya kuwawezesha watunga sera kuelewa utafiti waliofanya na kutumia matokeo hayo kusaidia kwenye maendeleo ya nchi kwa kuboresha sera zilizopo au kutunga mpya kupitia ushahidi huo wa kisayansi walioupata.

"Watunga sera wana mambo mengi hawana muda wa kusoma andiko la kurasa kumi tena lenye maneno ya kisayansi ambalo halijafsiriwa kwa lugha nyepesi wao kuelewa hivyo kupitia maachapisho madogo ya kisera yaliyotafsiriwa vizuri yatawezesha

*Inaendelea Uk. 22*

watu hao kuyasoma na kuyatumia kwa faida ya Taifa na jamii kuliko kuyatumia tuu kupata shahada" alieleza Prof. Mabiki.

Mada mbalimbali ziliwasilishwa ikiwemo kuandika andiko vuziri la kuomba fedha za utafiti,Maombi bora ya ruzuku na utekelezaji wake,Kuelewa usimamizi wa kuandika tafiti na uchapishaji,uwasilishawaji wa chapisho la kisayansi kwajili ya kuchapishwa,mrejesho na namna ya kujibu mawazo kutoka kwa mpitiaji na nyingine nyingi ambazo ziliwasilishwa na Dkt. Alcardo Alex Barakabitze,Prof. Faith Mabiki, Dkt. Rose Kicheleri, Dkt. Offoro Kimambo, Dkt. Elly Ligate, Dkt. Nkuba Nyerere, Dkt. Emmy SolomonLema.

Mafunzo hayo ya siku mbili yalibeba kauli mbiu isemayo kuandika kwa maendeleo endelevu, ukazaji, usimamizi na ujengaji uwezo wa SUA kwenye kuandika maandiko ya machapisho na Ruzuku.

*Baadhi ya picha za wanafunzi wa Shahada za Juu wa kozi mbalimbali katika Ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi.*


















***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (kushoto) akielezea jambo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mwananchi Communications Limited (MCL) Bw. Bakari Machumu ambaye pia ni Mhitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo***

# *SUA yajivunia Machumu, Mkurugenzi wa MCL*

*Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinaendelea kujivunia kuwa na wahitimu bora wenye uwezo na kutoa mchango chanya katika jamii.*

*Bakari Machumu, mhitimu wa Shahada ya Kilimo Ndaki ya Kilimo wa mwaka 1998 ni mmoja wa wanafunzi ambao walihitimu masomo yao SUA ambaye anaendelea kuipeperusha vyema bendera ya Chuo hicho ambapo Jumamosi ya tarehe 08.03.2024, ameingia kwenye rekodi ya kumhoji Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

*Mahojiano hayo aliyafanya katika tukio la TheCitizen RisingWomen lililoandaliwa na magazeti ya MCL ambapo Machumu anafanya kazi hapo kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mwananchi Communications Limited (MCL).*

*Kufanya vizuri kwa Machumu kunaendelea kukitangaza vyema Chuo ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.*




**Ardhi ni Hazina**



# Wanawake SUA watakiwa kuwa kitu kimoja na kusaidiana

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Mipango, Utawala na Fedha Prof. Amandus Muhairwa amewataka Wanawake wa Chuo hicho kuwa kitu kimoja na kusaidiana kwa dhati wao kwa wao pindi linapotokea tatizo la aina yoyote hasa la Unyanyasaji wa Kijinsia vilevile kuwasaidia vijana wao chuoni hapo kwa kuwa wao ni kina mama na walezi hivyo wanachukua nafasi ya kwanza na ni rahisi kufikiwa.


Alibainisha hayo wakati akizungumza na wanawake hao kwenye hafla fupi ya kilele cha Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika katika ukumbi wa Multipurpose Kampasi ya Edward Moringe mjini Morogoro ambapo amesema jambo la muhimu litakalo onesha ushirikiano wao ni kuhakikisha hawatalifumbia macho na kulinyamazia suala la unyanyasaji wa kijinsia.

Prof. Muhairwa aliwataka wanawake hao kulitumia Dawati la Jinsia lililoanzishwa chuoni hapo kufikisha malalamiko yao na kuwa wa kweli na wawazi pindi wanapolitumia Dawati hilo na si kulitumia kama mlango wa kuangamiza wengine na endapo wakiweza kupeleka malalamiko yao katika Dawati la Jinsia chuoni hapo ana uhakika kuwa watakuwa wamefikisha ujumbe sehemu sahihi kwa kuwa SUA ina Dawati lenye nguvu ambalo halikuchaguliwa kiholela lakini pia lina watu waliobobea na wenye uwezo mkubwa katika kazi.

Aidha alisema ikiwa kwa namna yoyote suala lao haliwezi kupitia kwenye dawati hilo bado kuna njia mbalimbali za kutumia ikiwemo kuwatumia watu wazima waliopo katika taasisi hiyo kwa kuwa hakuna nyumba inayokosa watu wazima hivyo wanaweza kuwafuata na kuwafikishia taarifa zao zaidi.

Awali kabla ya hafla hiyo Dkt. Charles Moses Lyimo ambaye ni Mratibu wa Utekelezaji wa Sera za Jinsia SUA wakati akizungumza na SUAMEDIA alisema SUA ni miongozi mwa Taasisi zinazolinda na kupigania haki za kijinsia kwa pande zote ikiwemo haki ya mwanamke mahali pa kazi, na kwamba wanahitaji mazingira salama ili kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi.

Aliongeza kwa kuitaka jamii nzima ya Tanzania kuweza kutambua nafasi ya mwanamke ambaye amekuwa ni mzazi, mlezi vilevile ni mwalimu wa kwanza katika kutoa maarifa hivyo wakiitambua nafasi yake na wakatoa ushirikiano wa maarifa na uchumi nchi itaweza kupiga hatua kubwa.



> "Unapofika Vyuo Vikuu utakuta watoto wa kike wanajitenga katika fani ambazo kwa bahati mbaya huku mtaani hazilipi vizuri sana"

# Wanafunzi wa kike wajengewe uwezo katika masomo ya Sayansi

*Imeelezwa kuwa kutokuwepo kwa wanafunzi wengi wa kike wanaosoma masomo ya sayansi, teknolojia na uhandisi katika Vyuo vikuu nchini kunatokana na wanafunzi hao kutojengewa uwezo katika hatua za awali na hivyo kuona kuwa masomo hayo ni kwa ajili ya wanafunzi wa kiume pekee.*

*Hayo yalielezwa na Profesa Msaidizi John Jeckoniah kutoka Idara ya Taaluma za Maendeleo na Mafunzo Mkakati SUA wakati akizungumza na SUA Media katika mafunzo ya kuwajengea uwezo Wanataaluma wa SUA kuhusu mbinu za kuboresha ufundishaji kwa Wanataaluma hao yanayofanyika kwa siku nne mjini Morogoro.*

*Prof. Jeckoniah alisema wazazi, walezi, walimu pamoja na jamii kwa ujumla wanapaswa kuwajengea uwezo watoto wa kike na kutambua kuwa wao wapo sawa na watoto wa kiume na wana uwezo wa kusoma na kufanya kazi zinazohusisha sayansi na teknolojia ambayo ndiyo mwelekeo wa mapinduzi ya kisayansi katika Dunia ya sasa.*

*"Unapokuja Vyuo vikuu utakuta watoto wa kike wanajitenga katika fani ambazo kwa bahati mbaya huku mtaani hazilipi vizuri sana au zinawaelekeza kwenye majukumu yao ya kimsingi kwenye ule mgawanyo wa majukumu ya msingi ya kimila na kitamaduni, hatupati wanafunzi wengi wa kike kwenye masomo ya sayansi sio kwa sababu hawajui bali tu ni kwa sababu hawajajengewa uwezo hasa wanapofika kidato cha pili kwenye suala la uchaguzi wa masomo",*
*alisema Prof. Jeckoniah.*



# SUA yaendelea na mpango wake wa kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuimarisha utendaji kazi

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeendelea na mpango wake wa kutoa mafunzo kwa watumishi mbalimbali ili kuimarisha utendaji kazi wa pamoja kwa watumishi wa Taasisi hiyo ambao utaleta tija na ufanisi kwa wafanyakazi na taifa kwa ujumla.

Akizungumza na SUA Media Machi 22, 2024 chuoni hapo katika mafunzo ya kikao kazi cha Maafisa Utumishi na Watendaji katika Ofisi za Menejimenti ya Chuo hicho Afisa Tawala Mkuu Peter Mwakiluma alisema mpango huo ulikuwepo kwa muda mrefu lakini pia ni utekelezaji wa maelekezo ya Tume ya Utumishi wa Umma wa kutaka yafanyike mafunzo ya aina hiyo.

"Chanzo cha mafunzo haya kwanza ni mpango ambao ulikuwepo kwa muda mrefu lakini pia kwa sababu tunafanyiwa ukaguzi na Tume ya Utumishi wa Umma kama Taasisi na utendaji kazi kwa ujumla tulipokaguliwa tulikumbushwa kwamba tunahitaji kuwa na huu utaratibu kwa sababu kuna maeneo ambayo tulifanya vizuri sana na yale yaliyohitaji maboresho kama haya ya kuwa na umoja zaidi katika kufanya kazi ndiyo tukaona tuanze kuhusisha wafanyakazi moja kwa moja", alisema Mwakiluma.

Akielezea sababu ya mafunzo hayo kufanyika kwa watumishi wa Idara ya Utawala na Maafisa Utumishi, alisema watumishi hao ndiyo wasimamizi wa masuala ya utawala katika Chuo hivyo wana jukumu la kufikisha ujumbe kwa watendaji wengine wa namna ya kuimarisha utendaji kazi kwa kushirikiana pamoja.

"Mafunzo haya yamekuja wakati muafaka zaidi kwa sababu yameongozana na utaratibu mpya wa kutathimini wafanyakazi ambao zamani ilikuwa OPRAS lakini sasa hivi tumeenda kwenye mfumo wa PEPMIS ambapo kila mtumishi anatathiminiwa kila siku kutokana na utendaji wake, kwa hiyo ukiunganisha na haya mafunzo ya kuboresha utendaji kazi utaona umuhimu wake katika suala la kuwa na umoja zaidi", alisema Mwakiluma.




**MAKTABA YA TAIFA YA SOKOINE YA KILIMO**

**Jarida limetolewa na:**
Kitengo cha Mawasiliano na Masoko
S.L.P 3000, Chuo Kikuu, Morogoro, Tanzania
**Simu:** 255-023-2640006/7/8/9,
**Baruapepe:** communicationandmarketing@sua.ac.tz